JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

IMETHIBITISHWA ISO 9001:2015

# TAARIFA KWA UMMA

## KUONGEZA MUDA WA KUTUMA MAOMBI YA UTOAJI WA HUDUMA YA USAMBAZAJI NA URUSHAJI WA MAUDHUI YA REDIO KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA KIDIJITALI (DIGITAL RADIO MULTIPLEXER) T-DAB+ NA DRM30

1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2003 yenye jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano ya Kielektroniki na Posta nchini Tanzania.

2. TCRA inatoa taarifa kwa umma juu ya upatikanaji wa teknolojia ya kidijitali ijulikanayo kama "Digital Sound Broadcasting – DSB" kwa ajili ya kurusha maudhui ya utangazaji wa redio hapa nchini. Hivyo inakaribisha maombi kwa wenye nia ya kutoa huduma ya urushaji wa maudhui ya redio kwa kutumia T-DAB+ na DRM30 (Digital Radio Multiplexer).

3. Kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za Utoaji Leseni, Tangazo la Serikali Na.422 la mwaka 2014, TCRA imeainisha Masafa (174-230 MHz) na (525-1605 kHz) kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Maudhui ya redio kwa kutumia teknolojia ya T-DAB+ na DRM30 mtawalia katika kila eneo la huduma (Service Area). Ili kuongeza ufanisi katika matumizi ya masafa, TCRA kwa sasa imepanga kila eneo la huduma litakuwa na mtoa huduma binafsi (private) mmoja atakayepewa leseni. Hivyo dirisha la maombi ya leseni ya urushaji wa maudhui ya redio kwa kutumia T-DAB+ na DRM30 limefunguliwa katika maeneo yafuatayo:-

   **A. Maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya Huduma ya kurusha Maudhui kwa kutumia Teknolojia ya T-DAB+/ DRM30 ni kama ifuatavyo: -**

| Na. | Eneo la Huduma | Idadi ya watoa huduma (Digital Radio Multiplexers) |
|---|---|---|
| 1. | ARUSHA | 1 |
| 2. | DAR ES SALAAM | 1 |
| 3. | DODOMA | 1 |
| 4. | MBEYA | 1 |
| 5. | MWANZA | 1 |

4. Waombaji wanatakiwa kuzingatia **Mwongozo** wa uwasilishaji wa maombi ya utoaji wa huduma ya usambazaji na urushaji wa maudhui ya redio kwa kutumia teknolojia ya kidijitali ya redio unaopatikana katika tovuti ya TCRA: www.tcra.go.tz.

5. Maombi yote ya utoaji wa huduma tajwa hapo juu yawasilishwe kwa kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao ***Tanzanite Portal*** kupitia kiunganishi kifuatacho: https://tanzanite.tcra.go.tz kabla ama ifikapo tarehe **16 Agosti 2025.**

6. Tafadhali zingatia kwamba, endapo waombaji katika eneo fulani la huduma wako zaidi ya mmoja, ***TCRA itaweka Masafa ya eneo husika katika mchakato wa ushindani, yaani zabuni / Mnada***.

7. Waombaji watakaoingia kwenye ***mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa ili waweze kuwasilisha zabuni zao katika bahasha iliyofungwa ambayo itafunguliwa mbele ya wazabuni wote***.

8. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa hayatafanyiwa kazi.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,
Mawasiliano Towers,
20 Barabara ya Sam Nujoma,
S. L. P. 474,
**14414 DAR ES SALAAM**.

Imetolewa Tarehe **16 Juni 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Mon Jun 16 22:22:05 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**